JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Anwani ya simu "AFYA", **DODOMA**
Simu nambari: **255 26 2323**
Fax: 2137591
(Barua zote ziandikwe kwa
Katibu Mkuu)

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Kitivo cha Sanaa na Sayansi
ya maendeleo ya Jamii,
S.L.P. 743,
Jengo na 11
DODOMA.

Kumb. Na. JB/87/522/ 08/ 82 **05 April, 2017**

Wakuu wa vyuo,
Vyuo vya Sayansi Shiriki za Afya,
Tanzania Bara.

YAH: TAARIFA YA KUFANYIKA KWA MITIHANI YA KITAIFA YA MARUDIO (SUPPLEMENTARY EXAMINATIONS) IFIKAPO MWEZI AUGUSTI-OKTOBA, 2017

Rejea mada iliyotajwa hapo juu.

Tangu kumalizika kwa mitihani ya kitaifa iliyokuwa inaendelea kuanzia tarehe 27 Februari hadi 30 Marchi.Wizara imekuwa ikipokea barua kutoka kwa baadhi ya Wanafunzi wakiwa wamepitia katika uongozi wa vyuo vyao wakiomba kupewa tena mitihani ya marudio kwa mara ya pili baadaya kufanya vibaya mitihani yao.

Pamoja na maombi yote yaliyopokelewa, ni vyema kuelewa kwamba wizara ina utaratibu wa kutoa mitihani ya kitaifa mara mbili tu kwa mwaka, yaani wakati wa kipindi cha mwezi Februari-Marchi na Augusti-Oktoba kila mwaka.

Mitihani ya kitaifa inayotolewa vipindi hivyo ndiyo inayotumika kutahini wanafunzi wanaofanya mitihani yao kwa mara ya kwanza (First Sitting) na wale wanaorudia mitihani (Supplementary Examinations) baada ya kufanya vibaya wakati wa mitihani ya awali.

Kwa barua hii ninawaelekeza muwaandae wanafunzi wote wanaotakiwa kufanya mitihani ya marudio ili waweze kuwa tayari kufanya mitihani yao wakati wa mitihani ya kitaifa inayotarajiwa kufanyika wakati wa kipindi cha mwezi **Augusti-Oktoba 2017**. Aidha, ni vyema muwasisitize kwamba wanatakiwa kujiandaa vyema kwani iwapo watashindwa kufaulu mitihani ya marudio kwa mara ya pili wataondolewa masomoni **(Discontinue from Studies)** na hawatapewa tena nafasi ya kurudia masomo yao.

Ninasisitiza kwamba wakuu wa vyuo wote tumieni taarifa hii kuwaelekeza vyema wanafunzi wenu na kuwaepusha wasitumie muda wao na rasilimali zao nyingi kusafiri kuja wizarani kwa ajili ya kuomba kupatiwa mitihani ya marudio.

Ni matumaini yangu kwamba maelekezo haya yatazingatiwa na kuvisaidia vyuo kuweka utaratibu sahihi utakaowawezesha wanafunzi wote wanaosubiri kurudia mitihani kurejea vyuoni walau wiki nane (8) kabla ya mitihani kuanza kwa ajili ya maandalizi.

Ninawatakia kila la kheri katika usimamizi wa uendeshaji mafunzo.

Dkt. Otilia F.Gowelle
K.n.y: KATIBU MKUU (AFYA)

Nakala:
Katibu Mtendaji,
NACTE
S.L.P. 7109,
DAR ES SALAAM.